

## **HABARI MUHIMU KUHUSU MANUFAA YA BIMA YAKO YA MEDICAID.**

### **Tafadhali Chukua Hatua Mara Moja**

Tunaandika ili kukupa habari muhimu kuhusu manufaa ya bima yako ya Medicaid. Kama inavyohitajika na sheria ya nchi, Jimbo la Rhode Island linatekeleza shughuli ya usasishaji wa ustahiki wa bima ya Medicaid ili kuthibitisha kwamba kila mtu anayepokea bima ya Medicaid anaendelea kustahiki. Rekodi zetu zinaonyesha kwamba una hali maalum zinazoathiri ustahiki wako.

#### **Muda wa matumizi ya Bima yako ya Medicaid Unaisha**

Maeleo tulio nayo kutoka kwa Idara ya Watoto, Vijana na Familia (Department of Children, Youth, and Families, DCYF) ya Rhode Island inayonyesha kwamba hustahiki tena kupokea bima ya Medicaid.

#### **Jinsi ya Kutambua Ikiwa Unaweza Kuendelea Kupokea Bima ya Medicaid**

Ikiwa ungependa kuendelea kupokea bima ya Medicaid, tunakuhimiza utume ombi ili tuweze kubainisha ikiwa unastahiki. Ili utume ombi, lazima ujaze Fomu ya Maombi ya Msaada ya DHS-2. Unaweza kufanya hivyo:

- **Mtandaoni:** Tembelea [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov) na ubofye kitufe cha "Get Started" (Anza) chini ya sehemu ya "Apply for Health and Human Services Programs" (Tuma Ombi la Mipango ya Idara ya Afya na Huduma za Binadamu).
- **Kwa barua:** Pakua fomu ya maombi ya DHS-2 katika [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov), jaza fomu ya maombi na uiwasilishe kwa Rhode Island Department of Human Services, P.O. Box 8709, Cranston, Rhode Island 02920-8787.

- **Ana kwa ana:** Weka fomu yako ya maombi ya DHS-2 uliyojaza katika kisanduku cha barua katika ofisi yoyote ya DHS. Tafuta ofisi ya DHS iliyo karibu nawe katika [www.dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices](http://www.dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices).
- **Kwa simu:** Wasiliana na DHS kwa nambari 1-855-697-4347 ili ujaze fomu yako ya maombi ya DHS-2 kwa simu.

Usichelewe. Tuma ombi la bima ya Medicaid Mara moja ili tuweze kubainisha ikiwa unastahiki kuendelea kupokea bima.

#### **Unachowenza Kufanya Ikiwa Ombi Lako la Medicaid Limekataliwa**

Baada ya kushughulikia ombi lako, utapokea Notisi ya Uamuzi wa Manufaa (Benefit Decision Notice). Notisi hii itakufahamisha ikiwa bima yako ya Medicaid imeidhinishwa au imekataliwa. Ukinyimwa bima, Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako itakufahamisha kuhusu chaguo nyingine za kuendelea kupokea huduma ya bima.

- Ikiwa unastahiki kupokea bima ya HealthSource RI inayofadhiliwa na Jimbo kwa miezi miwili, Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako itajumuisha maelezo haya.
- Ikiwa hukubali uamuzi wetu kuhusu manufaa yako, unaweza kukata rufaa kwa kufuata utaratibu ulioelezwa kwenye Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako.

Tembelea [www.staycovered.ri.gov](http://www.staycovered.ri.gov) ili upate maelezo zaidi kuhusu ustahiki wa kupokea bima ya Medicaid na jinsi ya kuomba msaada.